*International Journal of Arts and Education 1(4):33-44, June 2017*

© SERIAL PUBLISHERS, 2017 www. serialpublishers.com

# KINAYA KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI: MFANO WA TAMTHILIA YA *MSTAHIKI MEYA*

FRIDAH Oiko Gesare[1], Dkt JAMES Ontieri Omari[2], Dkt. EMMANUEl Kisurulia Simiyu[3]

[1]Mwanafunzi, Chuo Kikuu cha Maasai Mara- Kenya
[2]Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Maasai Mara- Kenya
[3]Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Kabianga- Kenya

**Barua pepe:** oikofridah2012@gmail.com2012@gmail.com, jontieri@gmail.com, Kisurulia@gmail.com

**Ikisiri:** Mwandishi wa kazi ya fasihi kama mzawa wa jamii anayoindikia, huwa na mbinu mbalimbali za kisanaa anazoweza kutumia katika kuwasilisha mawazo yake kama anavyoyashuhudia katika jamii. Mbinu hizi ni nyingi na hivyo mwandishi hulazimika kufanya uchaguzi wa ile itakayofaa ujumbe anaowasilisha. Uchaguzi huu huathiriwa na jinsi anavyotaka mawazo yake kueleweka na kuleta taathira anayokusudia. Aidha mbinu anayoteua mwandishi sharti iwe ni ile isiyotinga mahusiano ya wanajamii (watawala na watawaliwa). Mojawapo ya mbinu hizo ni kinaya. Kinaya ni mbinu ya kisanaa ambayo hulenga kukuza mawazo kwa njia iliyo kinyume na matarajio. Makala haya yametathmini matumizi ya kinaya katika kukejeli viongozi wa nchi changa za Bara la Afrika ambao katika utendaji kazi duni ambao umezalisha maendeleo yasiyokuwepo. Makala haya yameongozwa nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Makala haya yamebainisha kwamba Arege ameegemea sana mtindo wa kinaya katika kuwasilisha mawazo yake. Imebainika pia kuwa lengo kuu la kinaya ni kusuta kwa lengo la kuadilisha wanajamii katika kuimarisha viwango vya maendeleo yanayohitajika katika katika sekta mbalimbali. Aidha, kupitia kwa makala haya imebainika kuwa Arege ameegemea sana kinaya ili kukejeli jamii nzima bila kuhujumu mahusiano ya kitabaka yaliyomo katika jamii anayoiandikia. Makala haya yamezingatia kinaya kwa kuegemea nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo.

**Istilahi za Kimsingi:** Kinaya, Kejeli, Mtindo na Uwasilishaji wa mawazo

## 1.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo iliyoasisiwa na Leech (1969). Nadharia hii kimsingi hujishughulisha na mbinu za kiisimu na zile za kifasihi katika kuchunguza matini. Aidha inajikita katika kuangalia kinachosemwa (mtindo) na zaidi huchunguza ni kwa jinsi gani kinavyosemwa (mtindo). Kwa mantiki hii mtindo ni uti wa mgongo katika uelewekaji wa kazi ya fasihi kwa kuwa ni kigezo maarufu kinachosaidia katika kubeba ujumbe wa mtunzi. Na hii inatokana na ukweli kuwa kazi ya fasihi hueleweka vyema kwa kuchunguza lugha iliyotumika kuisuka (Leech, 1969) Hivyo basi nadharia hii huchunguza zaidi jinsi lugha ilivyotumika katika muktadha fulani ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi.

## 1.1 Utangulizi

Mtindo wa uwasilishaji wa mawazo ni mbinu za kimtindo ambazo mwandishi huzitumia kuyadokeza tu mawazo katika matini za fasihi. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007) mtindo wa uwasilishaji wa mawazo hutupa uwezo wa kuyajua mawazo ya mwandishi na wahusika. Hii hutusaidia kufahamu mbinu ya kimsingi ya kuyaelezea hayo mawazo (maudhui). Hivyo basi kuwasilisha mawazo ni suala la uamuzi wa mwandishi ambalo huhusu mbinu anazotumia kuelezea maudhui yake. Wamitila (2002) anayaeleza maudhui kwamba ni jumla ya masuala na mambo yanayozungumziwa katika matini za kifasihi. Maudhui huhusu ujumbe ambao mwandishi anajadili katika kazi za fasihi. Mwandishi hawezi kuwa na mtindo bila ya kuwa na cha kueleza na vivyo hivyo hawezi kuwa na cha kueleza bila kuwa na mtindo wa kukieleza . Hii ina maana kuwa mtindo na maudhui ni vitu vinavyotegemeana na kukamilishana katika kuleta maana. Hivyo basi hatuwezi kamwe kupuuza maudhui kila tunapochunguza mtindo. Ni kupitia kwa mtindo ambapo mtunzi wa kazi za fasihi huwasilisha maudhui yake. Mtindo ndio humwezesha mwandishi kuwa na upekee katika kushughulikia mada husika na kuifanya kuonekana mpya hata kama imekwishaandikiwa na watunzi wengine, (Leech, 2007). Arege ni mwandishi ambaye ameegemea mbinu ya kinaya katika kuwasilisha ujumbe katika uandishi wake. Tumechunguza jinsi Arege alivyowasilisha maudhui kwa kinaya ili kuwakejeli Waafrika ambao licha ya kudai kuwa huru, hawaelekei kuelewa dhana hii na ndicho chanzo cha wao kushindwa kujisimamia katika misingi ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni.

Makala haya yanalenga kubainisha matumizi ya kinaya katika kukejeli viongozi ambao wameshindwa kuwaelekeza wananchi ili kupata maendeleo yanayohitajika katika kusukuma jamii mbele. Mwandishi ametalii asasi mbalimbali ili kuonyesha ukweli wa uozo huo akitumia mtindo wa kinaya. Kinaya kama mbinu ya kisanaa haijashughulikiwa kwa mapana kama zilivyo mbinu zingine k.v. isitiari na taswira. Wahakiki wengi katika fasihi huihusisha tu kama kipengele cha kimtindo bila kuitolea maelezo ya kina ama wengine hawaitaji kabisa katika tahakiki zao. Hali hii imechangiwa na wengi kuichukulia kinaya sawa na mzaha.

## 1.2 Tofauti na uhusiano kati ya Kinaya na Kejeli

Kinaya ni mbinu ambayo huelezea mambo kinyume na matarajio ya wahusika au jamii. Kwa mujibu wa Wales (1989) kinaya hutokea wakati maneno yanayotumiwa huleta mkinzano kimaana katika muktadha tofauti na ilivyokusudiwa na msomaji. Maelezo haya yanaashiria kuwa kinaya huhitaji muktadha fulani ili kuifafanua kwa nia ya kuleta maana iliyokusudiwa. Ndiposa kamusi ya Wales (2001) inasisitiza muktadha kama kigezo maalum ili kufafanua kinaya. Kinaya inaelezwa kuwa ni maneno yanayotumiwa kwa mkinzano na maana inayohitajika katika muktadha maalum au i nayokusudiwa na mwandishi, msemaji ama mtumiaji.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2008) kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Kinaya huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi ambavyo mambo yanaonekana na jinsi yalivyo sasa (uhalisia wake). Kwa upande mwingine, Kuhenga (1977) anafafanua kejeli kuwa ni uneni wa kimafumbo ambao hulenga kumuudhi mtu kwa nia ya kumwonya kichinichini bila bughudha. Japo kuna tofauti katika ya kinaya na kejeli kutokana na maelezo ya Mbatiah na Kuhenga (keshatajwa), Wamitila (2008, 2003, 2002), Senkoro (2011), Msokile (1993) na Mrikaria (2010) wanaona kinaya kuwa sawa na kejeli.

Mbatiah (2001) anakubali maoni ya Wataalamu hawa ambapo anaeleza kejeli au kijembe kuwa ni matamshi yanayolenga kumtweza mtu kwa sababu huwa ya kuchoma, kukata na kutia uchungu. Mtu anapopewa sifa ambazo hastahili, basi huwa anakejeliwa. Ingawa Mbatiah (keshatajwa) anakubali kuwa kejeli huchukuliwa kuwa kisawe cha kinaya, anasisitizwa kuwa kejeli ni aina ya kinaya yenye ukali wa kipekee. Maoni ya Mbatiah (2001) na ambayo makala haya yameegemea yanaieleza kejeli kama aina ya kinaya kwa kuwa ni kupitia kwa kinaya ambapo kejeli huweza kufahamika. Maoni ya Mbatiah (keshatajwa) ndiyo yanayoendelezwa na Giora (2001) ambaye anaeleza kwamba kinaya hailengi kwenye nia ya msemaji ilhali kejeli hulenga. Anaeleza zaidi kuwa kinaya huhitaji muktadha wa kiufafanuzi tofauti na kejeli. Hii ndiyo sababu Giora (1997) anasema kuwa maana ya kinaya kama ilivyotumika katika matini huwa ngumu kuifafanua.

Muktadha wa kiufafanuzi ni jukwaa la mawasiliano baina ya msomaji na mwandishi ili kufahamu ujumbe. Na hii ndiyo sababu ya Short (1996) kuelezea kinaya kama ushirikiano wa siri kati ya mwandishi au msemaji na msomaji, msikilizaji au hadhira. Hii pia inabainisha kuwa, tofauti na zilivyo mbinu zingine k.v. methali, tashbihi na takriri; kinaya humhitaji msomaji kusoma kwa kina kazi ya fasihi naili kuitambua. Haya ndiyo yanayorejelewa na Schaffer (1982: 15) anaposema:

> Utambuzi wa kinaya haupo katika maneno yenyewe… bali hutokana na ishara za muktadha wa mazungumzo au kutokana na mawasiliano ya msemaji. (Tafsiri Yetu)

Hivyo basi kinaya hujitokeza na kupata ufafanuzi katika muktadha maalum. Hii hufanya kinaya kuwa tofauti na mbinu zingine za kisanaa kwa kuwa msemaji anaweza kukataa au kupinga alichokisema kuliko maelezo ya moja kwa moja ambayo hutolewa na mbinu zingine za kisanaa (Haiman, 1990).

Katika makala haya kinaya ni ile inayojikita katika kuelezea kinyume cha matarajio katika muktadha wa kijamii. Makala yanabainisha namna kinaya ilivyotumika kukejeli (kukashifu) viongozi na watawaliwa kwa kiasi fulani kupitia kwa taasisi mbalimbali za kijamii. Tumetumia kinaya kurejelea hali inayozua mkinzano wa maana ya kinyume na kejeli kwa nia ya kukashifu mawazo ya kinaya. Kwa hivyo tumeichukulia kejeli kama sehemu ya kinaya.

### 1.3 Mipaka ya Makala

Kinaya ni kipengele cha kimtindo ambacho hutumiwa na waandishi katika vipera vyote vya fasihi, iwe simulizi au andishi ili kuwasilisha mawazo yao kwa njia inayoibua maana tofauti na ile inayowasilishwa. Hata hivyo matumizi yake hutegemea zaidi kipera husika na mawazo anayoyawasilisha mwandishi. Makala haya yamejikita katika tamthilia ya Arege ya *Mstahiki Meya* (2009).

## 2.0 Muhtasari wa tamthilia ya Mstahiki Meya

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni mojawapo ya kazi za Arege ambazo zinaweka wazi chimbuko la uongozi wa kiimla uliotukuka barani Afrika. Tamthilia hii inazungumzia maisha ya wanacheneo ambao wanaongozwa na Mstahiki Meya ambaye anaitwa Sosi. Mstahiki Meya ni kielelezo cha viongozi wa kiimla katika nchi kadha changa za bara la Afrika. Cheneo ni kielelezo cha nchi za

bara la Afrika ambazo zilipata uhuru na hivyo nyadhifa za uongozi zikatwaliwa na viongozi wa Kiafrika wenye uwezo hafifu. Sosi kama kiongozi, licha ya kuchaguliwa mara tatu amejawa na tamaa na ubinafsi wa kujitakia makuu na hivyo kushindwa kushughulikia mahitaji ya waliomchagua (wananchi). Meya Sosi hapendwi na wanacheneo kutokana na utendaji duni katika kusuluhisha matatizo yanayoikumba jamii ya wanacheneo licha ya yeye kudai kuwa mapenzi ya wanacheneo ndiyo chanzo cha kuchaguliwa mara tatu mfululizo. Kugutuka kwa wafanyikazi katika sekta mbalimbali kunasababisha migomo na mwishowe Sosi anavuliwa uongozi aliojitapa nao. Inakuwa kinaya kwani alikuwa amedai kuwa ataongoza milele.

## 2.1 Kinaya katika Tamthilia ya *Mstahiki Meya*

Arege ametumia mtindo wa kinaya katika kukashifu au kukejeli viongozi wa nchi changa za Bara la Afrika ambao wanazinaendesha kwa tamaa ya kujilimbikia mali licha ya wananchi kuwachagua kwa imani ya kutetea maslahi yao. Makala haya yamechunguza jinsi kinaya inavyojitokeza katika huduma za taasisi mbalimbali za kijamii kama ifuatavyo:

### 2.1.1 Kinaya katika uongozi

Neno uongozi limetokana na kitenzi 'ongoza' ambacho kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21 kinaelezewa kuwa ni kuwa mbele ili kuonyesha mwelekeo fulani. Inaendelea kueleza kuwa kuongoza ni kusimamia shughuli na kuonyesha jinsi ya kufanya jambo. Kulingana na maelezo haya ni wazi kuwa jukumu la viongozi ni kuwaelekeza wananchi au wanaowatawala kwa njia ambayo itawawezesha kupata maendeleo katika jamii Maendeleo haya hujitokeza katika huduma mbalimbali za kijamii kama vile; afya, elimu na ajira, mahakama, na dini. Madai haya ni kinaya kwani Msathiki Meya ambaye hapendelei jina lake halisi- Sosi, badala ya kuwaongoza wanacheneo ili kupata maendeleo anajishughulisha na masuala ya kumfaa mwenyewe pamoja na wale wanaomdanganya. Meya Sosi ni kielelezo cha viongozi wasio na mwelekeo wa maono ya kusababisha maendeleo katika uongozi wao. Badala ya kuunda sheria zilizohusiana na matakwa ya wanacheneo, amefuata mtindo wa kikoloni kwa lengo la kujinufaisha kama ilivyoonyeshwa na Orwell katika riwaya yake ya *Shamba la Wanyama* kuwa Mkimwa ambaye anatwaa hatamu za uongozi baada ya wanyama kuungana na kufaulu kumfurusha Bw. Mtiki (binadamu aliyewanyanyasa wanyama) alisaidiwa na nguruwe wenye tamaa kama yeye katika kubadilisha sheria zilizoundwa na Bwana Mtiki kwa manufaa yao binafsi. Kwa kifupi, viongozi hawa wanaendeleza na kudumisha uongozi wa kiimla ambao ulianzishwa na ukoloni mkongwe. Lengo la Arege ni kukejeli uwezo duni wa viongozi wa nchi ambao ni chanzo cha kukosa maendeleo katika taasisi mbalimbali za kijamii. Ni kama anavyoeleza Orwell (keshatajwa) katika riwaya yake ya *Shamba la Wanyama* kuwa baada ya wanyama kuungana pamoja na kufanya mapinduzi yaliyomfurusha Bw. Mtiki kutoka shamba lao, binadamu ambaye aliwadhulumu, nguruwe walipochukua hatamu za uongozi wanakuwa wakatili hata zaidi kumshinda binadamu aliyekwishafukuzwa.

Viongozi wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali hawana haja na mahitaji ya wanajamii. Viongozi hawa wamemiliki mbinu mbalimbali za kuwadanganya wananchi kiasi cha kuwafanya waamini kuwa wanayashughulikia majanga yanayowakumba. Wanacheneo wengi wanaamini uongo huu na wale wachache wanaoonekana kujua njama hizi hupuuzwa au kukemewa vikali kama vile Diwani III na Dkt. Siki. Imani hii imewafanya wakazi wa Cheneo kuendelea kudidimia katika ulitima. Kwa kuwa wakazi hawa ni maskini walio na uhitaji wa hali ya juu, viongozi hupata

fursa ya kuwadhalilisha kwani mhitaji kila wakati atasalia kuwa mtumwa katika jamii hii iliyojengeka kwenye misingi kibinafsi. Tunafahamu kuwa dawa zilizotumainiwa kufika hospitalini hazitawasili. Matamshi ya Meya yanadhihirisha ukweli huu anaposema:

> Ahadi zetu zimetufaa hadi sasa. Atajua nani ukweli ila wenyewe myaseme huko nje? (uk. 21)

Matamshi ya Meya kama kiongozi yanadhihirisha uongozi ambao huna mwelekeo au tuseme ulioshindwa kutimiza lengo lake la kimsingi. Ni kinaya kwa kuwa licha ya Meya kuaminiwa kuwa anayashughulikia majanga yao anatoa matamshi kama haya. Ukweli ni kuwa uongozi wa kidikteta badala ya kuimarisha viwango vya maisha, umesababisha viwango duni vya maendeleo katika mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa kutojali wananchi wake. Hii ni mojawapo ya mbinu ambazo viongozi hutumia ili kupata nguvu na uhalalisho wa kuendelea kusalia uongozini kwani huwapa wananchi matumaini yasiyozalisha maendeleo yoyote katika nchi. Matokeo yake ni kuzorota kwa maendeleo ya nchi zao kinyume na maendeleo yanayotarajiwa. Hivi ndivyo Arege anavyofaulu kuwakejeli viongozi wanaowahadaa wananchi kuwachagua katika nyadhifa mbalimbali. Kwa mtindo huu mwandishi anakejeli viongozi kwa kumezwa na tamaa inayokuza ubinafsi dhidi ya shabaha ya kimsingi ya wananchi wanaolenga kuongozwa ili kufanikisha maendeleo.

### 2.1.2 Kinaya katika dhima ya Washauri na Ushauri

Kamusi ya Oxford (2008) inaeleza kuwa mshauri ni mtu ambaye hutoa ushauri kwa kuwa ana maarifa na ujuzi kuhusiana na taaluma husika. Maelezo haya yanaonyesha kuwa mshauri ni sharti awe na ujuzi katika taaluma anayoshughulikia ili aweze kuwa na manufaa. Hata hivyo, katika tamthilia ya Mstahiki Meya hali hii ni kinyume.

Kwa kinaya, mwandishi anatalii na kukejeli dhima ya washauri na ushauri wao katika mataifa machanga. Ameonyesha na kuweka wazi ni kwa jinsi gani ushauri unaotolewa ni muhimu katika kuleta au kukosesha maendeleo katika nchi za bara la Afrika. Ushauri wa kupotosha wanaopata viongozi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu ni chanzo cha maangamizi ya kiuchumi yanayoshuhudiwa katika nchi hizi. Kupitia kwa ushauri wa Madiwani I na II na Bili, wanacheneo wanaendelea kuteseka na kudidimia katika maisha ya ulitima. Badala ya kumshauri Meya aweze kuunda sera mwafaka za kuimarisha maendeleo ya Cheneo, wanamshawishi na kumfumba macho kutokana na ukweli wa hali ya Cheneo mradi tu wanufaike. Wanamsaidia kwa kufanya mipango ya kuifisidi Cheneo kwa manufaa yao tu. Bili anapoona kuwa hamna njia mwafaka itakayomwezesha kunufaika anatoa ushauri wa kuuza fimbo ya Meya jambo ambalo linakubaliwa kwa pamoja na Diwani Wa I na II (washauri wa Mega). Haya yote hayaonyeshi chochote chenye manufaa kwa wananchi bali ubinafsi na ndiposa inakuwa ni kinaya.

Meya Sosi anajua na kufahamu fika kuwa hana uwezo wa kuongoza manispaa ya mji wa Cheneo. Licha ya kufahamu hili inakuwa kinaya kwa kuwa anawaajiri washauri ambao inasadifu kuwa hawana tajriba ya kumsaidia katika kuliongoza Baraza la Cheneo. Matokeo yake yanakuwa maangamizi na mateso kwa wanacheneo.

### 2.1.3 Kinaya katika vyombo vya Dola

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011) polisi ni askari wa kulinda usalama. Hii huhakikisha kwamba wananchi wanaweza kutekeleza shughuli za kujenga nchi bila woga. Katika mazingira ya Cheneo, polisi ni walinzi wa *Mstahiki Meya* na vibarakala wake. Badala ya kuwatumika wanacheneo, askari hawa wanawadhulumu kwa kuwapiga na kuwaumiza kila wanapoandamana kwa nia ya kulalamikia au kushtakia majanga yao. Askari kwa uhitaji wao, hawana budi kupokea na kutekeleza amri zinazowadhalilisha wananchi kutoka kwa vikaragosi wa Meya mradi wahakikishe kuwa wana riziki. Askari wanajua fika dhima yao ya kuwalinda wananchi lakini kwa kuwa ni amri wao hutekeleza madhila haya kwani wanaogopa adhabu itakayozalikana kutokana na ghadhabu ya Mstahiki Meya. Askari badala ya kuwahakikishia wanacheneo usalama, wanazua rabsha na kuwaumiza na hata zaidi kusababisha vifo kwa wananchi wasio na hatia. Hiki ni kinaya. Ushahidi huu unajitokeza Diwani III anaposema:

> … Haya ya watu kuvurumizwa na askari wanapotaka kushtakia hali zao. Mji si mji tena. Askari wameutwaa. Hata mimi nimeona vigumu kuingia humo wakati wafanyikazi wetu wanafurushw. (uk. 47)

Mahakama au korti ni mahali ambapo kesi husikilizwa na hakimu au jaji na kuitolea uamuzi (Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja 2011). Katika mahakama tunataraji haki kutendwa kwa misingi ya Sheria za kikatiba. Hali hii ni kinaya katika tamthilia ya Mstahiki Meya kwa kuwa Meya ambaye ndiye anayefaa kutetea haki ndiye anakuwa katika mstari wa mbele katika kuvunja sheria huku akijua kuwa mahakama itamtetea. Meya anaposhtakiwa kortini na Mwanakandarasi aliyemfuta kabla ya muda wake kukamilika, badala ya kufungwa anaibuka kwa na faida kwani atanufaika na fidia atakayolipwa mwanakandarasi huyu. Haya yote ni kutokana na mipango murua ya wakili wa baraza na mshauri wake Bili.

### 2.1.4 Kinaya katika Dini

Dini ni nguzo ya kimsingi na maarufu inayohimili jamii katika misingi ya maadili. Mahubiri na maombi ya kidini hustahili kusifu kadhia ambazo huendeleza utu katika jamii. Umuhimu wa maombi ni kusuta vitendo viovu na visivyofaa ambavyo ni chanzo cha uozo katika jamii. Na ndio sababu inaaminiwa kuwa jukumu la kimsingi la dini ni kuwapa watu mwongozo wa kimaadili katika mazingira ya kibinafsi na pia ya kijamii. Hivyo basi dini ina jukumu la kujenga maadili katika jamii na kuhakikisha utendaji wa haki na usawa.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* dini inatumika kwa kinaya kuwatakasa viongozi waovu kwa umma mkubwa sawia na vyombo vya habari. Inakuwa kinaya kwamba wahubiri kama viongozi hawa wanaowatakasa, hudhihirisha tamaa na ubinafsi kwani wao pia hushiriki katika kuyafilisisha mataifa yao. Kwa kukubali kuhongwa kinyume na dhima yao ya kimsingi ya kuwakemea na kuwasuta viongozi wanaoendeleza uongozi ulioandamwa na tamaa iliyojengeka kwenye ubinafsi, inakuwa kinaya kwani hatutaraji kuwaona wakitekeleza vitendo kama hivyo. Viongozi wa kidini kwa ngozi ya kondoo, hutumia uwezo wao katika kuwahadaa viongozi kwa tamaa na ubinafsi wa kujiendeleza. Wao hawana budi kupokea hongo kwa fumbo la sadaka kwani wamejawa na tamaa na ubinafsi. Licha ya kujua kuwa uongozi wa Meya una doa

linalowaumiza wanacheneo katika sekta zote za kiuchumi, mhubiri anamwombea ili uongozi wake udumu akisema hivi: Mwondolee nuksi ya maadui na kinyongo cha mahasidi (uk. 42). Hata hivyo, kinaya zaidi katika maombi haya ni kwamba maadui na mahasidi wanaorejelewa na Mhubiri katika muktadha huu ni wanacheneo na wafanyikazi wanaopinga njama za uongozi unaowafaa wachache katika jamii. Wanaopinga uongozi mbaya wa Meya ni wazalendo kama Daktari Siki na Kheri (Diwani III). Kwa mkabala huu Arege anafaulu kukejeli na hivyo kuikashifu dhima ya kimsingi ya dini ambayo badala ya kutunza maadili inatukuza maangamizi kutokana na ubinafsi wa kujitakia makuu.

### 2.1.5 Kinaya katika Vyombo vya Habari

Kijamii, vyombo vya habari vimepewa au kutwikwa jukumu la kusambaza habari kwa faida na maendeleo ya wananchi. Hii ina maana kuwa vyombo vya habari ni taasisi ya kuwahudumia wananchi wote kwani ni mali na manufaa yao. Hii haimaanishi kwamba taasisi zingine k.v. elimu, ajira, dini n.k. si muhimu katika kuendeleza nchi bali ni kutambua dhima yake ya kimsingi katika kukuza taasisi hizi. Vyombo vya habari vina jukumu la kumpasha mwananchi habari kuhusu hali halisi ya maendeleo aliyopata ama kukosa kupata. Kwa njia hii, mwananchi hupata fursa ya kujithamini na kujikosoa ili aweze kujiimarisha kimaendeleo. Hata hivyo ili vyombo hivi viweze kuafikiana na dhima yao, ni sharti viweze kufichua na kuweka wazi utendaji kazi wa serikali katika juhudi za kuhamasisha au kukwamiza maendeleo bila mapendeleo. Ni muhimu pia kwa vyombo vya habari kuwaruhusu wananchi katika kutoa maoni yao na kusikika na viongozi wao. Haya yote yatawezekana kama vyombo hivi vitahudumu vikiwa huru na bila ushawishi kutoka kwa serikali. Kwa njia hii vyombo vya habari vitaaminika na wote.

Katika mazingira ya tamthilia ya *Mstahiki Meya,* vyombo vya habari havitumiki kueneza habari za kuhamasisha maendeleo ya Cheneo badala yake vinatumika kueneza propaganda za uongo ambazo zinawasababishia wanacheneo hali ngumu kimaisha. Tena badala ya vyombo hivi kuhudumu kwa manufaa ya wanacheneo, vinamhudumia matakwa ya Meya. Taka zinapotapakaa mji mzima baada ya mgomo wa wafanyikazi kwa malipo duni, vyombo vya habari vinatumika kutangaza habari za kuwaajiri vijana waliohitimu bali hawana kazi kama njia ya kuwaadhibu waliogoma ifuatavyo:

> **Diwani 1:** Tunaweza kutangaza katika vyombo vya habari. Pia tunaweza kutumia vipaza sauti kuwatangazia vijana wasio na ajira. Watu wengi huko nje wana njaa. (uk.73)

Hili si suluhu kwa vijana ambao hawana kazi, badala yake ni kuwapumbaza kwani wao pia hawatanufaika katika ajira wanazoitiwa. Hivyo basi vyombo vya habari havitekelezi jukumu lake la kimsingi la kumpasha mwanachi habari za ukweli bali vyombo hivi vinamdhalilisha kwa kueneza habari za uongo zisizomfaidi chochote. Hiki ni kinyume cha matarajio. Ni kinaya kwani vyombo vya habari havitekelezi majukumu yao ya kimsingi ya kuimarisha maendeleo kama inavyotakiwa. Aidha, mwandishi anatumia kinaya ili kukejeli viongozi wanaotumia vyombo vya habari kwa manufaa yao pekee dhidi ya nchi nzima. Hali hii ndiyo inayoua imani kwa vyombo vya habari kutoka kwa wananchi. Kwa kinaya, taasisi ya vyombo vya habari inakejeliwa kwa kutotumia vyombo hivyo kupasha wananchi maswala yanayohamasisha maendeleo katika jamii.

## 2.1.6 Kinaya katika Ofisi za Serikali

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011) ofisi ni chumba ambapo wafanyikazi hukaa na kuhudumia watu. Kwa mantiki hii, ofisi ni mahala pa kufanyia shughuli muhimu za kuleta maendeleo katika jamii. Ofisi ni mahali ambapo tunataraji kuwaona wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali katika uongozi wakijadili hatua wanazonuia kuchukua kwa manufaa ya wananchi. Katika mazingira ya tamthilia hii, inakuwa kinaya kwani ofisi ni mahali pa kufanyia shughuli za kuifisidi serikali na kujinufaisha kibinafsi. Meya na madiwani wake ambao pia ni kitengo cha washauri, wanapanga njama za kulifisidi Baraza Cheneo pasina kujali maslahi ya wanacheneo wanaowawakilisha katika nyadhifa wanazozishikilia. Inakuwa ni kinaya kwamba shughuli za kuyafisidi mataifa yao kwa rasilimali ndizo huongoza mipango na majadiliano katika ofisi ambapo tunataraji kuwaona viongozi na washikadau mbalimbali wakijadili maswala ya kusababisha maendeleo kwa manufaa ya wananchi. Kwa mfano, Meya Sosi akiwa afisini badala ya kuwazia namna ya kusuluhisha matatizo yanayotinga maendeleo, anawaza masuala yanayoporomosha Cheneo kama inavyodhirika katika uzungumzi nafsia ufuatao:

> Safi! (*kimya*) Safi! Huyu nitamfurusha. Hatamu mpya na mipango mipya. Hata akishitaki ni bure. (Anafungua kurasa kadha huku akiuchunguza kila ukurasa kwa makini. Anaufikai ukurasa fulani ambao unavuta nadhari yake. Anatabasamu.) Hali ni shwari kabisa. Nitawapa mapokezi ya kupigiwa mfano. Hoteli ya kifahari. Vyakula kutoka kila utamaduni duniani. Sisembe. La hasha! Mvinyo nitauagiza kutoka Urusi na divai divai kutoka Ufaransa… (uk. 25)

Kutokana na jinsi anavyowaza Meya, tunabaini kuwa ukoloni mkongwe bado ungali katika mataifa ya Afrika licha ya kudai kuwa yako huru. Mwandishi ametumia uzungumzi nafsia huu kwa kinaya ili kuwakejeli viongozi mataifa ya Afrika ambao licha ya wananchi wanaowaongoza kuishi katika ulitima na uhitaji mkubwa, wanaweza kuwapa mapokezi ya kifahari wakoloni wanaowafadhili. Ukuruba huu unajionyesha katika tamthilia ya *Amezidi* ambapo mwandishi anawakejeli wahusika wake Ame na Zidi ambao wanaishi katika pango. Licha ya kuonyesha uhitaji mkubwa katika maisha yao, katika onyesho linalofuata wanajikuta katika utajiri usiokuwepo na wa vyombo vya thamani vyote vilivyoagizwa kutoka nchi za kigeni. Huu ni ubadhirifu wa rasilimali ambazo zingeweza kuwafaa wakazi wao ambao wanadidimia katika ulitima usiokadirika kinyume na wanvyowaza wanacheneo.

Meya ni kiwakilishi cha viongozi ambao hutumia misaada wanayopokea kwa njia mbaya pasina kunufaisha wananchi walio masikini. Misaada inayopewa mataifa haya fukara, haitumiwi kuyaendeleza bali kuwateka nyara viongozi hawa ambao huburura mataifa yao kwa ufukara zaidi kwa kuitumia kujionyesha. Meya anatumia misaada hii kuwaandalia wafadhili wake mapokezi ambayo yamezidi uwezo wake ilmradi aonekane mkarimu. Mwandishi anasisitiza kuwa maendeleo hayatapatikana katika kutegemea misaada ambayo Mohamed anaiita ‘paja lililooza’ bali katika kuwaza na kutenda haki. Aidha, mwandishi anadhihaki uwajibikaji duni unaoonekana kwa viongozi katika mataifa machanga.

### 2.1.7 Kinaya katika ugavi wa Ardhi

Ardhi ni jambo ambalo limekuwa likizozaniwa katika jamii mbalimbali kwa muda mrefu. Kila wakati baada ya uchaguzi, wananchi wana ilhamu kubwa ya kuona viongozi wakilitatua suala zima kuhusiana na ardhi. Kwa hivyo ni matarajio ya wananchi kuwa viongozi wanaowawakilisha katika nyadhifa mbalimbali watatafuta suluhu la kudumu katika umiliki na ugavi sawa wa ardhi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa kuna haki katika umiliki wa ardhi. Inakuwa ni kinaya kwamba viongozi na wale wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali za kuwahudumia wanajamii ndio huhakikisha kuwa wanapata ardhi kwa mbinu zozote zile bila kuwajali walala hoi wasiomiliki chochote. Bili ana vipande vya ardhi alivyopata kutokana na ukupe wake kwa Meya. Meya vilevile ana vipande kadha vya ardhi. Vipande hivi wamevipata kwa njia zisizo halali. Bili amevipata vipande vyake kutokana na juhudi za ukupe wake kwa Meya. Hili ni dhihirisho kuwa licha ya mataifa ya ulimwengu wa tatu kupiga vita ukatili ili kuleta usawa kwa watu wa matabaka tofauti, ukaragosi uliokithiri katika jamii unakwamiza juhudi hizi na kukatiza tamaa. Vipande hivi vya ardhi vinastahili kuwafaa wananchi wote haya hivyo ni kinaya kuwa havimfai yeyote katika jamii kwa kuwa ni mali ya kibinafsi. Hii inadhihirika wazi kutokana na matamshi ya Meya ifuatavyo:

> Nisipokuwa nazo nani atakuwa nazo? Mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Nimebakiza vitano *incase*. Wewe nilikugawia vine. Unaweza kuuza kimoja au viwili kwa ajili hiyo vingine viweke kwa ajili yao hao watoto unaowahangaikia, hasa ile *prime plot*. (uk. 27)

Vipande walivyo navyo ni mali, lakini kwa sasa wamevinyakua kwa manufaa yao wenyewe na aila zao. Hii ni kinaya ikizingatiwa kuwa mali ya umma hulengwa kufaidi wananchi wote na vilevile kuimarisha maendeleo katika sekta zote dhidi ya manufaa ya wachache.

### 2.1.8 Kinaya katika Elimu na Ajira

Kamusi ya Oxford (2008) inaelezea elimu kama mchakato wa kutoa au kupokea mafunzo fulani au maarifa, kwa kazi. Kwa vyovyote vile elimu ni muhimu katika kuleta maendeleo katika nchi yoyote. Maelezo haya yanaenda sambamba na maoni ya Ilhan (2001) anayesema hivi:

> '… Hamna jamii yoyote ambaye imepata kuendelea pasina kuwekeza katika kuelimisha watu wake…'

Maelezo haya yanaashiria kuwa kuwekeza katika elimu ya jamii ambayo ina malengo ya kuendeleza nchi dhidi ya kuipokea tu. Kinachobainika wazi ni kuwa upataji wa elimu si muhimu bali ni upataji wa elimu inayoendana na mahitaji ya kijamii. Licha ya umuhimu huu, elimu katika jumuiya ya Mstahiki Meya haichukuliwi katika uzito unaofaa. Meya Sosi anafahamu fika kuwa viwango vya elimu ni duni. Ni matarajio yetu kuwa kama kiongozi ataweka wazi mikakati ya kuimarisha viwango vya elimu na zaidi iendane na mahitaji ya jamii. Inakuwa kinaya kuwa badala ya Meya kushughulikia jangamoto katika sekta ya elimu anawapeleka watoto wake ng'ambo akidai kuwa viwango vya masomo ni duni. Anasema haya:

> *'… siku ile nilikuambia hawasomei hapa tena. Viwango viko chini kidogo.' (uk. 26)*

inakuwa kinaya kwani hatutaraji matamshi kama haya kutoka kwa kiongozi tunayetumaini kuwa anasuluhisha matatizo yanayoikumba sekta ya elimu. Hata hivyo mwandishi anafaulu kukejeli viongozi waliokosa maono ya katika kuendeleza nchi zao kwenye misingi ya elimu.

Elimu anayopata mwanajamii itakuwa na manufaa ikiwa itamwezesha kuitumikia jamii katika sekta mbalimbali. Hii huwezekana tu ikiwa inaendana na mahitaji ya jamii husika. Katika Tamthilia ya Mstahiki Meya, inakuwa ni kinaya kuwa vijana waliohitimu hawana kazi na wale wanaobahatika kupata kazi za kijungu jiko wanashindwa kutimiza mahitaji yao. Badala ya Meya Sosi kubuni mikakati ya kuwapa ajira vijana waliohitimu ili walete maendeleo, anawatumia kama tishio kwa wafanyikazi waliogoma. Anasema hivi:

> Kuna vijana wengi wasio na kazi ilhali wamehitimu kutoka vyuo vikuu Fresh kabisa. Wanaoleta siasa wapewe barua za kuwatimua na kuwakumbusha kuwa kazi wanazofanya si za bali ni Baraza bali ni za Baraza la Cheneo. (uk. 21)

Ni matumaini ya wanajamii kila wanapowachagua viongozi kwamba watashughulikia suala la elimu na ajira kwa wanajamii. Kwa hakika hii ni mbinu mojawapo wanayotumia kujizolea kura kutoka kwa wananchi. Utawasikia wakisema hivi wakati wa kampeni: *'mkinichagua kama kiongozi wenu nitahakikisha kuwa kila mtoto ameelimika na kuhakikisha kwamba nimebuni sera ili kuzidisha ajira kwa vijana.'* Lakini kutokana na matamshi hayo hapo juu inakuwa ni kinaya. Hili si suluhu kwa ukosefu wa ajira bali ni ishara ya utepetevu katika kukabiliana na changamoto katika sekta ya elimu.

**Hitimisho**

Ukweli ni kuwa tamthilia nzima imesimuliwa kwa mtindo wa kinaya na mwandishi akiwa na lengo la kukejeli viongozi wa mataifa machanga katika vitendo vyao viovu vinavyozuia maendeleo ya kiuchumi pamoja na yale ya kijamii licha ya kumtafakarisha msomaji. Tumechunguza kinaya katika tamthilia ya Mstahiki Meya na kubaini kuwa licha ya kufafanua ujumbe, kinaya hutumika kuisuta jamii kwa kuikejeli ili irekebishe mienendo mibaya kwa nia ya kuendeleza maadili ambayo ni msingi wa maendeleo katika jamii. Aidha, imebainika kuwa kinaya kama mojawapo ya mtindo wa uwasilishaji mawazo hutekeleza dhima ya kumtafakarisha msomaji ili aweze kutumia tajriba yake ya kifikra ili kuibua maana ya kazi ya fasihi. Kwa njia hii, kinaya hukaribisha kazi ya fasihi na kuileta karibu na uhalisia. Pia imebainika wazi kwamba kinaya inahusishwa na tamathali zingine kama vile kejeli, dhihaka na tashtiti. Mjadala unaweza kuendelezwa hapa ili kukuza uchambuzi huu na kuiweka mbinu hii katika misingi ya kueleweka.

**Marejeleo**

Giora, R. (1997). Understanding Figurative and Literal Language: The graded salience Hypothesis. *Cognitive Linguistics, 8*(3), 183-206.

Giora, R. (2001). Masking One's themes: Irony and politics of indirectness. In M. M. Louwerse & W. van Peer (Eds.), *Thematics in Psychology and literacy studies (pp.283-300).* Amsterdam: John Benjamins.

Haiman, J. (1990). Sarcasm as theater: *Cognitive linguistics, 1*(2), 183-203.

Ilhan, O. (2001). *Role of Education in Economic Development: A Theoretical Perspective*. https://mpra.ub.uni.muenchen.de/9023.

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2011). *Toleo la pili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi za Kiswahili.* Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Leech, G. (1969). *A linguistic Guide to Modern English Poetry*. Essex: Longman Group Ltd.

Leech, G. & Short, M. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to Fictional Prose*: New York: Longman Limited.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing Ltd.

Mrikaria, E. S. (2007). Kejeli katika Fasihi ya Kiswahili- Tanzania. *Katika Swahili Forum nambari 14, Uk.197-206*. Chama cha Masomo ya Kiafrika.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers Ltd.

Mohamed, S.A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

O.U.P. (2008). *The Oxford Advanced Learners English Dictionary*. (Toleo la 8). Oxford University Press.

Scaffer, R. R. ( 1982). Vocal Clues for Iron in English. *Unpublished Ph.D thesis*. University of Oihio State.

Senkoro, F. E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.

Short, M. (1996). *Exploring the language of Poems, Plays and Prose*. London: Longman Publishers Limited.

Orwell, G. (1988). *Shamba la Wanyama*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wales, K. (1989). *A Dictionary of Stylistics*. London: Longman PublishersGroup.

Wales, K. (2001). *A Dictionary of Stylistics*. United Kingdom. Pearson Education Limited.

Wamitila, K. W. (2002*). Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003*). Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Focus Publications Limited.